

# HALMASHAURI YA MJI HANDENI



## SHULE YA SEKONDARI KWENJUGO

Kumb . Na. HTC/52836/J10/15 14/12/2020

Jina la mwanafunzi: .....

S.L.P. ....

.....

### **YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KWENJUGO WILAYA HANDENI MKOA TANGA**

1.0 Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha **KWANZA** katika shule hii **mwaka 2021**. Shule ya Sekondari Kwenjugo ipo umbali wa km 2 Kaskazini mwa mji wa Chanika wilayani Handeni.

Muhula wa kwanza wa kimasomo utanza tarehe **11/01/2020**. Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe hiyo bila kukosa, vinginevyo utapoteza nafasi hiyo muhimu katika maisha.

### **2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia:**

#### **2.1 Sare ya shule:**

- [a] Sare ya shule hii ni suruali mbili-rangi ya **Bluu Bahari** na mashati mawili- meupe ya mikono mifupi kwa wanaume.
- [b] Sketi mbili- rangi ya **Bluu Bahari** na mashati mawili- meupe ya mikono mifupi kwa wasichana.
- [c] Kwa watakaovaa hijabu- rangi ya hijabu ifanane na **shati la shule**.
- [d] Viatu vyeusi visivyo na visigino virefu- kwa wavulana na wasichana
- [e] Soksi nyeupe kwa wavulana na wasichana
- [f] Sare ya michezo na kazi za nje ni T-Shirt [fulana] ya **kijivu** ya mikono mifupi.

#### **2.2: Sheria na kanuni muhimu za shule hii ni:**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

- [a] Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

- [b] Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu
- [c] Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni [preparation]
- [d] kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- [e] Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- [f] Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
- [g] Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- [h] Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- [i] Kuwasiliana/kuzungumza **KIINGEREZA** wakati wote unapokuwa katika **MAZINGIRA YA SHULE**.

### **2.3: Makosa yafuatayo yanaweza yakasababisha ukafukuzwa shule:**

- [1] Wizi
- [2] Uasharati na ushoga
- [3] Ubakaji
- [4] Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile: uvutaji

bangi,cocaine,mirungi,kubeli,sigara n.k

- [5] Kupigana au kupiga au kutishia kupiga.
- [6] Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- [7] Kudharau bendera ya taifa
- [8] Kuoia au kuolewa
- [9] Kupata mimba au kusababisha mimba ndani au nje ya shule.
- [10] Kutoa mimba
- [11] Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- [12] Kukataa adhabu kwa makusudi.
- [13] Mwanafunzi kuwa na **SIMU YA MKONONI**.

### **3.0: Mambo mengine muhimu:**

**Fomu zifuatazo zijazwe na kurudishwa kwa Mkuu wa Shule mwanafunzi anaripoti shuleni.**

- [a] Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii ikabidhiwe kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
- [b] Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Fomu hii ijazwe na mwanafunzi mwenyewe.
- [c] Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria,kanuni na taratibu za shule.

### **4.0: Tafadhari soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

.....

(J.A.ABDURABI)

**MKUU WA SHULE**

KWENJUGO SECONDARY SCHOOL

**MEDICAL CERTIFICATE FORM**

To be completed by medical officer in respect of form I/V entrants

Pupils full name:.....

Age:.....

Blood count(red and white):.....

Stool:.....

Urinalysis:.....

Syphilis test:.....

T.B Test:.....

Ears:.....

Chest:.....

Spleen:.....

Abdomen:.....

ADDITIONAL INFORMATION: eg. Physical defects or impairments, infections, chronic or family diseases etc.

.....  
.....  
.....

I certify the above is fit /unfit admission into a secondary school

Designation:.....

Station:.....

Date:.....

Official stamp